

JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA

KURUGENZI YA MAWASILIANO YA RAIS IKULU

Simu: 255-262961500/1
Nukushi: 255-262961502
Baruapepe : press@ikulu.go.tz
Tovuti : www.ikulu.go.tz



OFISI YA RAIS,
IKULU,
1 BARABARA YA JULIUS NYERERE,
CHAMWINO,
S.L.P 1102,
40400 DODOMA.

01 Septemba, 2024

Dar es Salaam

TAARIFA KWA VYOMBO VYA HABARI

Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na Amiri Jeshi Mkuu, Mhe. Dkt. Samia Suluhu Hassan amesema katika kipindi cha miaka 60, Jeshi la Ulinzi la Wananchi wa Tanzania (JWTZ) limehakikisha ulinzi wa mipaka, limekuwa kimbilio la wananchi na kuwa mstari wa mbele pindi wananchi wanapokabiliwa na changamoto mbalimbali ikiwemo majanga ya asili au ajali.

Rais Dkt. Samia amesema hayo leo wakati wa kilele cha Maadhimisho ya Miaka 60 ya JWTZ yaliyofanyika katika Uwanja wa Uhuru.

Rais Dkt. Samia amebainisha kuwa katika kipindi cha uhai wa JWTZ, imetimiza wajibu na majukumu yake kikamilifu kwa ujasiri, uhodari na ufanisi mkubwa na hivyo kuendelea kuwa Jeshi la ulinzi, ukombozi na kioo katika harakati za ukombozi wa Afrika na kulinda amani duniani, kama ilivyokuwa misingi ya kuanzishwa kwake.

Rais Dkt. Samia amesema JWTZ imekuwa kinara katika kutafsiri Dira, Sera na Mipango ya Serikali katika awamu zote za uongozi, na pia limegusa maisha ya wananchi kwa kutoa huduma za kijamii kama afya na elimu kwa kuendesha hospitali na shule kwa ambazo zinahudumia wanajeshi na raia.

Vile vile, Rais Dkt. Samia amelihakikishia Jeshi kuwa wananchi wanalipenda na kuliunga mkono Jeshi hilo na kwamba wananchi wamekuwa na mchango mkubwa katika mafanikio ya miaka 60 ya Jeshi hilo.

Rais Dkt. Samia amewasihi wananchi kuendelea kuliunga mkono Jeshi hilo kwa kudumisha amani na umoja wa kitaifa nchini. Aidha, amelihakikishia Jeshi utayari wa Serikali yake kushirikiana nalo katika kujenga Jeshi madhubuti zaidi, lenye zana za kisasa zaidi na lenye uwezo zaidi wa kuhimili na kukabiliana na changamoto mpya za kiulinzi na kiusalama.

A handwritten signature in blue ink, appearing to read "Sharifa B. Nyanga".

Sharifa B. Nyanga
Kaimu Mkurugenzi wa Mawasiliano ya Rais, Ikulu

